SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

## WIZARA YA VIJANA, AJIRA NA UWEZESHAJI

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA VIJANA, AJIRA NA UWEZESHAJI KWA MWAKA FEDHA 2026/2027

**ILIYOWASILISHWA NA**

**MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (MBM)**

**WAZIRI WA VIJANA, AJIRA NA UWEZESHAJI ZANZIBAR**

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**ZANZIBAR** **JUNI, 2026**

## WIZARA YA VIJANA, AJIRA NA UWEZESHAJI



***Mhe. Shaaban Ali Othman***
***Waziri wa Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji***
***Zanzibar***



***Mhe. Hassan Khamis Hafidh***
***Naibu Waziri wa Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji***
***Zanzibar***



***Salama Mbarouk Khatib***
***Katibu Mkuu***
***Wizara ya Vijana,***
***Ajira na Uwezeshaji***
***Zanzibar***



***Khalid Masoud Waziri***
***Naibu Katibu Mkuu***
***Wizara ya Vijana,***
***Ajira na Uwezeshaji***
***Zanzibar***

## YALIYOMO

*Mada* *Ukurasa*


**VIFUPISHO** ........ **iii**

**A. UTANGULIZI** ........ **1**

**B. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA VIJANA AJIRA NA UWEZESHAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026** ........ 5

**C. MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026** ........ **5**

- **MAPATO** ........ **5**
- **MATUMIZI** ........ **6**

**D. UTEKELEZAJI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026** ........ **7**

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIJANA** ........ **7**

**HALI HALISI YA VIJANA** ........ **7**

**PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA VIJANA** ........ **8**

**PROGRAMU NDOGO YA KUIMARISHA MABARAZA YA VIJANA** ........ **12**

**PROGRAMU YA URATIBU WA UPATIKANAJI WA AJIRA ZA STAHA KWA WOTE NA MAENDELEO YA USHIRIKA** ........ **14**

**PROGRAMU NDOGO YA AJIRA ZA STAHA KWA WOTE** ........ **14**

**PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI NA UIMARISHAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA** ........ **17**

**PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA** ........ **20**

**POGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI** ........ **20**

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA TAFITI ZA WIZARA** ........ **22**

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA** ........ **24**

**WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI** ........ **25**

**UPATIKANAJI WA FEDHA** ........ **25**

**UTEKELEZAJI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026** ........ **26**

**PROGRAMU KUU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI** ........ **26**

*Mada* *Ukurasa*

**PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA UTUMISHI YA WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI** ........ **29**

**PROGRAMU NDOGO YA UTUMISHI NA UENDESHAJI** ........ **29**

**PROGRAMU NDOGO YA AFISI YA URATIBU WA WAKALA PEMBA** ........ **31**

**E. CHANGAMOTO NA NJIA ZA UTATUZI** ........ **33**

**Utatuzi Wa Changamoto** ........ **34**

**F. MUELEKEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027** ........ **35**

**VIPAUMBELE VYA WIZARA** ........ **36**

**G. PROGRAMU ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027** ........ 37

**PROGRAMU KUU (P01): UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA** ........ **37**

**PROGRAMU KUU (P02): MAENDELEO YA VIJANA** ........ **38**

**PROGRAMU KUU (P03) URATIBU WA UPATIKANAJI WA AJIRA ZA STAHA KWA WOTE NA MAENDELEO YA USHIRIKA** ........ **40**

**WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI Fungu (105)** ........ **41**

**PROGRAMU KUU (P01) UENDESHAJI NA UTUMISHI WA WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI** ........ **42**

**PROGRAMU KUU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZANZIBAR (P02)** ... **43**

**H. SHUKRANI** ........ **44**

**I. HITIMISHO** ........ **47**

**MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027** ........ 47

- **MAPATO** ........ **47**
- **MATUMIZI** ........ 47

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| ADB | - | African Development Bank |
| BOA | - | Bank of Africa |
| BoT | - | Bank of Tanzania |
| COSTECH | - | Commission of Science and Technology |
| CUZA | - | Cooperative of Union of Zanzibar |
| DTB | - | Diamond Trust Bank |
| ILO | - | International Labour Organization |
| IRI | - | International Republican Institute |
| KOICA | - | Korean International Cooperation Agency |
| PBZ | - | People Bank of Zanzibar |
| SACCOS | - | Saving and Cradit Cooprative Societies |
| TADB | - | Tanzania Agrilcutrural Bank |
| UNDP | - | United Nations Development Programme |
| UNFPA | - | United Nations Fund for Population Activities |
| UNICEF | - | United Nations International Children Emergence Fund |
| YCI | - | Youth Challenge International |
| ILO | - | International Labour Organization |
| IOM | - | International Organization for Migration |

| | | |
|---|---|---|
| SEBEP | - | Skills Development for Youth Employability in Blue Economy Project |
| STATA | - | Statistical Analysis System |
| COMHESWA | - | Community Health Social Welfare in Africa |
| MoCU | - | Moshi Cooperative University |
| TCDC | - | Tanzania Cooperative Development Commission |
| CHAMAUTA | - | Chama cha Mazingira na Ufugaji Tija Tanzania |
| SACCOS | - | Savings and Credit Cooperative Societieties |
| VITAP | - | Vijana Tujenge Ajira kwa Pamoja |

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa, napenda kumshukuru **Mwenyezi Mungu**, mwingi wa Rehma na mwenye kurehemu kwa kutujaalia uhai, uzima na afya njema, tukaweza kukutana hapa kwa mara nyingine. Naomba **Allah (S.W)** aendelee kutudumisha katika Umoja, Amani, Utulivu, na Upendo kwani ndio nguzo thabit ya maendeleo ya Taifa letu.

2. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwapongeza kwa dhati viongozi wetu wakuu, **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushindi wao mkubwa katika uchaguzi Mkuu uliotokana na imani kubwa ya wananchi juu yao katika kusimamia na kudumisha Amani, Umoja, Utulivu, Mshikamano, kuulinda Muungano wetu na kutuletea maendeleo na hivyo wakaamua kuwachagua tena kutuongoza. Mwenyezi Mungu awazidishie afya njema, hikma, busara, uvumilivu na maisha marefu ili waendelee kutuongoza vyema.

3. **Mheshimiwa Spika,** Niwashukuru viongozi wetu hawa kwa maono na mitazamo yao kwani imeleta na inaendelea kuleta mabadiliko chanya ambayo sote tumekuwa mashahidi. Mifano mizuri ni kuimarika kwa huduma za jamii, miundombinu, mawasiliano na uwezeshaji wa wananchi

kiuchumi. Aidha kuanzisha Wizara za kuratibu na kusimamia changamoto za Vijana hasa ajira na kuwapatia maendeleo kwa kuanzisha Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji kwa Zanzibar na Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kwa Tanzania Bara.

4. **Mheshimiwa Spika,** Wizara hizi mbili zinashirikiana vizuri na ni mategemeo makubwa ya Serikali zetu zote mbili katika kuimarisha ushirikishwaji wa Vijana ambao wamefikia **asilimia 37.3** ya idadi ya watu Zanzibar, lakini pia wananchi kwa ujumla, katika kuwaletea Maendeleo na kukuza ustawi wao.

5. **Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima kubwa napenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa umahiri wake wa kuiongoza na kuisimamia nchi yetu kwa Amani na Utulivu pamoja na kusimamia vyema Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 – 2025 kwa mafanikio makubwa.

6. **Mheshimiwa Spika,** kipekee napenda kumpongeza **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla**, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar; kwa kuwa mstari wa mbele katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali na kutimiza azma na malengo ya kuiletea maendeleo Zanzibar na Wananchi wake.

7. **Mheshimiwa Spika,** napenda kukupongeza wewe binafsi, **Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid** Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Naibu Spika **Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma** pamoja na Wenyeviti wa Baraza **Mheshimiwa Dkt. Mahmoud Omar Hamad** na **Mheshimiwa Hudhaima Mbarak Tahir,** kwa kulisimamia na kuliongoza Baraza kwa hekima na umakini wa hali ya juu.

8. **Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru na kumpongeza, **Mheshimiwa Makame Mohamed Sufiani** Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Uwekezaji, **Mheshimiwa, Dkt. Mahmoud Omar Hamad** Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wote wa kamati hii kwa mashirikiano yao na miongozo ambayo imepelekea Wizara yetu kupata mafanikio makubwa kwa Vijana na Taifa kwa ujumla.

9. **Mheshimiwa Spika**, Kwa dhati kabisa, napenda kumpongeza **Mheshimiwa Hassan Khamis Hafidh**, Naibu Waziri Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji kwa msaada mkubwa anaonipatia katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yangu. Mheshimiwa Naibu Waziri amekuwa mstari wa mbele katika kufuatilia utekelezaji na kutoa miongozo na maelekezo kuhakikisha changamoto za utekelezaji wa Mipango ya Wizara inapatiwa ufumbuzi kwa wakati. Pia napenda kuwapongeza Waheshimiwa **Mawaziri** na **Manaibu Mawaziri** wote wa Serikali ya awamu ya nane

kwa kutekeleza majukumu ya Wizara zao vizuri na kuweza kupatikana kwa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi (**CCM**) **2020-2025**.

10. **Mheshimiwa Spika**, Kipekee, napenda kuwapongeza Watendaji wote wa Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji; Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Kaimu Afisa Mdhamini, Wakurugenzi, Katibu Mtendaji wa Baraza la Vijana, Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya ZEEA, Maafisa na Watendaji, Wananchi wenzangu hasa Vijana na washirika wa maendeleo kwa mashirikiano makubwa wanayonipatia katika kutekeleza mipango ya Wizara.

11. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuwapongeza Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa maelekezo wanayoyatoa kwa lengo la upatikanaji wa ufanisi katika Serikali ya awamu ya nane.

***Naomba hotuba hii iingie katika kumbukumbu ya Baraza lako tukufu pamoja na muhtasari huu, kama ilivyo katika kitabu kilichowasilishwa.***

12. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi huu, nakuomba uniruhusu niwasilishe kwa ufupi utekelezaji wa programu za Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026.

## B. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA VIJANA AJIRA NA UWEZESHAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

**13. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imetekeleza Programu kuu tatu ambazo ni:-

i. Programu ya Maendeleo ya Vijana;
ii. Programu ya Ajira za Staha na Maendeleo ya Ushirika; na
iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara.

## C. MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### MAPATO

**14. Mheshimiwa Spika,** Kwa wa fedha 2025/2026, Wizara ilipangiwa kukusanya **Shilingi 647,000,000** kati ya hizo Shilingi **550,000,000** Unguja na Shilingi **97,000,000** Pemba**.** Hadi kufikia Machi 2026, Jumla ya Shilingi **189,638,000** sawa na asilimia **38** zimefanikiwa kukusanywa kupitia Wizara ya Kazi na Uwekezaji. **Kiambatisho Nambari 1A** Kinafafanua zaidi**.**

**MATUMIZI**

15. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Vijana Ajira na Uwezeshaji, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ilikadiriwa kutumia **Shilingi 20,419,108,690** kati ya fedha hizo **Shilingi 1,133,095,000** mshahara, **Shilingi 2,786,013,690** matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi 16,500,000,000** ni kazi za Maendeleo.

16. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 Wizara ilikadiriwa kutumia **Shilingi 15,329,639,444** kati ya fedha hizo **Shilingi 849,821,251** mshahara, **Shilingi 2,104,818,193** matumizi ya kawaida na **Shilingi 12,375,000,000** ni kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, Wizara imeingiziwa **Shilingi 4,575,140,175** sawa na asilimia **30.** Kati ya hizo **Shilingi 754,627,447** sawa na asilimia **89** mshahara**, Shilingi 1,628,123,428** sawa na asilimia **77** matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi 2,192,389,300** sawa na asilimia **18** kazi za Maendeleo. **Kiambatisho Nambari 1B na 1C** Kinafafanua zaidi.

## D. UTEKELEZAJI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

17. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji halisi kwa kila programu ni kama ifuatavyo:-

### PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIJANA

18. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii, inajukumu la kuratibu na kuwajengea uwezo Vijana wa Zanzibar kujiimarisha kiuchumi, kijamii na kisiasa. Programu hii ina programu ndogo mbili; Programu ya Maendeleo ya Vijana na Programu ya Kuimarisha Mabaraza ya Vijana Zanzibar.

### HALI HALISI YA VIJANA

19. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Takwimu ya Sensa ya Watu na Makaazi ya Mwaka 2022, inaonesha kuwa Zanzibar ina idadi ya watu **1,889,773** kati ya hao vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35 ni **699,845** (Wanawake 368,066 na Wanaume 331,779) sawa na asilimia **37.3** ya idadi ya watu wote wa Zanzibar.

20. **Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar pamoja na Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar ya mwaka 2023 imeweka mikakati madhubuti ya kujenga mazingira rafiki na wezeshi kwa maendeleo na ustawi wa Vijana Nchini. Miongoni mwa mikakati hiyo ni kupunguza tatizo la ukosefu

wa ajira kutoka asilimia **19.7** kwa mwaka 2020/2021 hadi asilimia **10** kwa mwaka 2025/2026, Kuimarisha Sekta ya elimu na mafunzo ya amali, Huduma rafiki za Afya kwa Vijana, Stadi za Maisha, ujasiriamali, kilimo, uchumi wa buluu, Teknolojia ya habari na mawasiliano, Ubunifu, Usawa wa kijinsia, Uongozi, uzalendo, uwajibikaji, utamaduni, sanaa, Michezo, pamoja na ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana katika ngazi mbali mbali za maamuzi.

21. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa kufanya kazi wa mwaka 2024 Zanzibar, nguvu kazi ya vijana Zanzibar wenye umri wa miaka 15 - 35 ni **390,847** (Wanaume **216,270** na Wanawake **174,577**), kati ya hao Vijana **69,134** (Wanaume **22,366** na Wanawake **46,767**) sawa na asilimia **17.7** hawana ajira. Tatizo kubwa la ukosefu wa ajira limeonekana zaidi kwa Vijana wa Kike asilimia **26.8** ukilinganisha na Vijana wa Kiume asilimia **10.3** ya nguvu kazi.

## PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA VIJANA

22. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana**,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ilitengewa jumla ya **Shilingi 17,606,041,580** kati ya hizo **Shilingi 383,430,890** mshahara, **Shilingi 722,610,690** matumizi ya kawaida (Shilingi 360,000,000 kutoka Serikalini na Shilingi 362,610,690 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na **Shilingi 16,500,000,000** kwa Mradi wa maendeleo.

**23.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, **Shilingi 13,333,258,858** zilikadiriwa kutumika kati ya hizo **Shilingi 287,573,168** Mshahara, **Shilingi 670,685,690** matumizi ya kawaida (shilingi 308,075,000 kutoka Serikalini na shilingi 362,610,690 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na **Shilingi 12,375,000,000** miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, Programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana imeingiziwa **Shilingi 3,044,818,256** sawa na asilimia **23.** Kati ya hizo **Shilingi 229,432,116** sawa na asilimia **80** Mshahara, **Shilingi 622,996,840** matumizi ya kawaida (Shilingi 260,386,150 kutoka Serikalini na Shilingi 362,610,690 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia **93** na **shilingi 2,192,389,300** sawa na asilimia **18** mradi wa maendeleo.

**24.** **Mheshimiwa Spika,** Shughuli zilizotekelezwa kupitia programu hii ni kama zifuatavyo:-

i. Vijana **146,425** (Unguja 80,686 na Pemba 65,739) wakiwemo Wanawake 80,371 na Wanaume 66,054 wamepatiwa mafunzo ya Stadi za Maisha, Ujasiriamali, Stadi za Kazi, Afya ya Uzazi, Uongozi na Uzalendo, Ushiriki na Ushirikishwaji, Mabadiliko ya Tabia ya nchi, Amani na usalama na TEHAMA. **Kiambatisho namb 2A Kinafafanua.**

ii. Vikundi **66** vya vijana (17 Unguja na Pemba 49) vimepatiwa mikopo ya jumla ya **Shilingi 364,701,500** kwa ajili ya kujiendeleza katika shughuli za kiuchumi.

Mkopo huo ni kupitia Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar. Aidha, vikundi **48** (12 Unguja na Pemba 36 ) vimepatiwa vifaa vya uzalishaji kwa ajili ya kujiendeleza kiuchumi kupitia mradi wa Ujana Wangu Tunu Yangu unaotekelezwa na Shirika la Care International.

iii. Wizara kwa Kushirikiana na Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa. Kwa Mwaka 2026 Mbio hizo zimezinduliwa Mkoa wa Kusini Pemba na Mgeni Rasmi katika Uzinduzi huo alikuwa ni **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, chini ya Kaulimbiu isemayo "**Tanzania ni yetu sote, tushikamane kwa pamoja kuleta maendeleo**". Aidha Kilele cha mbio hizo kitafanyika tarehe 14 Oktoba 2026 Mkoani Rukwa, sambamba na Kumbukumbu ya Baba wa Taifa na Wiki ya Vijana kitaifa ambapo Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

iv. Wizara kwa mashirikiano na Washirika na Wadau wa Maendeleo ya Vijana Nchini, iliadhimisha Siku ya Vijana Kimataifa kwa lengo la kutambua thamani na nafasi ya Vijana katika Ujenzi na Maendeleo ya Nchi. Maadhimisho hayo hufanyika Duniani kote kila ifikapo tarehe 12

Agosti. Kwa Zanzibar, Mwaka 2025 yalifanyika katika ukumbi wa Skuli ya Utaani, Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.Mgeni Rasmi katika Kilele hicho alikuwa **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla** Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Zaidi ya Vijana **2,600** walishiriki katika shughuli mbalimbali zikiwemo; Ujenzi wa Taifa, Usafishaji wa Mazingira, Mabonanza ya Michezo pamoja na Makongamano ya kuhamasisha ushiriki wa vijana katika Uchaguzi pamoja na Utunzaji wa Amani. Ujumbe wa Kitaifa kwa Mwaka 2025 ulikuwa **"Wakati Wangu ni Sasa Nitashiriki Kuchagua na Kuchaguliwa Kwa Maendeleo Endelevu".**

v. Kupitia maadhimisho ya miaka 62 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi iliendelea kuhamasisha vijana katika Uzalendo, Amani na Umoja wa nchi yetu katika kuiletea maendeleo kwa kuendesha Kongamano lililoshirikisha Vijana **500** (Wanawake 279 na wanaume 221) kutoka Unguja na Pemba. Kongamano hilo lilibeba Ujumbe usemao **"Vijana Wazalendo, Ndio Nguzo ya Umoja, Amani na Maendeleo endelevu ya Zanzibar".** Mgeni rasmi katika Kongamano hilo alikuwa ni Mheshimiwa, Mudrik Ramadhan Soraga Waziri wa Mawasiliano Teknolojia ya Habari na Ubunifu.

25. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara kupitia Mradi wa Maendeleo ya Vijana imefanya manunuzi ya vifaa na vitendea kazi**.** Vifaa hivyo, vikiwemo Samani za Ofisi, vifaa vya TEHAMA, kilimo, ufugaji, ushoni na Vifaa vya ufundi wa aluminiam. Lengo ni kuimarisha Baraza la Vijana, Taasisi, Vituo vya Mafunzo na Vikundi vya kiuchumi vya Vijana. Taasisi na vituo **146** (Unguja 82 na Pemba 64) vitafaidika na mradi huu.

## PROGRAMU NDOGO YA KUIMARISHA MABARAZA YA VIJANA

26. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Baraza la Vijana**,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ilitengewa **Shilingi 654,461,110,** kati ya hizo **Shilingi 443,300,000** Ruzuku ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 211,161,110** ni Mshahara. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, **Shilingi 490,845,833** (Shilingi 332,475,000 Matumizi ya Kawaida na Shilingi 158,370,833 Mshahara) zilikadiriwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, Baraza la Vijana limeingiziwa **Shilingi 410,149,996** sawa na asilimia **84** kati ya hizo **Shilingi 156,083,556** sawa na asilimia **99** mshahara na **Shilingi 254,066,440** sawa na asilimia **76** matumizi ya kawaida.

27. **Mheshimiwa Spika,** Shughuli zilizotekelezwa kupitia programu hii ni kama zifuatavyo:-

i. Wizara kupitia Baraza la Vijana Zanzibar, imefanikiwa kuratibu na kusimamia Uchaguzi Mkuu wa Baraza la Vijana ngazi ya Shehia, Wilaya na Taifa. Viongozi **4,797** wamepatikana. Kati ya hao **4,656** ngazi ya Shehia, **132** ngazi ya Wilaya, na **9** kwa ngazi ya Taifa kwa Unguja na Pemba. Vijana wapya **1,321** (924 Wanawake na 397 Wanaume) walishajihishwa na kujiunga na Baraza la Vijana Zanzibar. **Kiambatisho nambari 2B kinafafanua.**

ii. Wizara kupitia Baraza la Vijana Zanzibar, imefanikisha ushiriki wa vijana **150,752** katika matukio ya kitaifa, kikanda na kimataifa yakiwemo; Upandaji wa Miti, Siku ya Vijana, Wiki ya Vijana na Mbio za Mwenge wa Uhuru na mikutano inayowajengea vijana uzalendo, uelewa wa haki za kiraia na fursa za kiuchumi.

## PROGRAMU YA URATIBU WA UPATIKANAJI WA AJIRA ZA STAHA KWA WOTE NA MAENDELEO YA USHIRIKA

28. **Mheshimiwa Spika,** Progamu hii ina programu ndogo mbili ambazo ni Programu Ndogo ya Ajira za Staha kwa wote na Programu ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika.

## PROGRAMU NDOGO YA AJIRA ZA STAHA KWA WOTE

29. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inajukumu la usimamizi wa Sera na Sheria za ajira, uratibu wa upatikanaji wa taarifa na huduma za ajira, uundaji na ukuzaji wa ajira za staha ndani na nje ya Nchi.

30. **Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa kufanya kazi wa mwaka 2024 Zanzibar, yameonesha nguvu kazi ya taifa ni **756,007** (Wanaume 421,496 na Wanawake 334,511) kati ya hao **82,683** (Wanaume 26,689 na Wanawake 55,993) sawa na asilimia **10.9** hawana ajira. Tatizo kubwa la ukosefu wa ajira limeonekana zaidi kwa Wanawake asilimia **16.7** ukilinganisha na Wanaume asilimia **6.3** ya nguvu kazi**.**

31. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu ndogo ya Ajira za Staha kwa wote**,** ilitengewa jumla ya **Shilingi 516,912,000** kati ya hizo **Shilingi 232,260,000** mshahara na **Shilingi 284,652,000** matumizi ya kawaida.

32. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Programu hii ilikadiriwa kutumia **Shilingi 330,918,000** (Shilingi 174,195,000 Mshahara na Shilingi 156,723,000 Matumizi ya Kawaida). Hadi kufikia Machi 2026, **Shilingi 303,775,350** ziliingizwa sawa na asilimia **92** kati ya hizo **Shilingi** 166,379,850 sawa na asimilia **96** zilitumika kwa mshahara na Shilingi 137,395,500 sawa na asilimia **88** kwa matumizi ya kawaida.

33. **Mheshimiwa Spika,** Shughuli zilizotekelezwa na programu hii ni kama zifuatavyo:-

    i. Wizara imeandaa rasimu ya Sheria ya Kuunda na Kukuza ajira na kuiwasilisha kwa wadau kutoka Taasisi za Serikali na Binafsi kupata maoni. Kwa sasa rasimu hiyo ipo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa lengo la kupata ushauri wa Kisheria.

    ii. Wizara kwa mashirikiano na Afisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Mahusiano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea na matayarisho ya Mkutano wa Pili wa masuala ya kazi kati ya Nchi za Baraza la Ushirikiano wa Nchi za Ghuba na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika unaotarajiwa kufanyika Nchini Tanzania tarehe 5 – 6 Oktoba, 2026.

    iii. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) imekusanya taarifa za uandaaji wa mfumo wa Taarifa za Soko la Ajira "Labour Market Information System".

Kwa sasa Shirika hilo limepanga kuleta wataalamu wa mafunzo na kuandaa mfumo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

iv. Vijana **10** (wanawake 8 na wanaume 2) walipatiwa hundi ya shilingi **37,200,000** katika shindano la matayarisho ya mpango wa biashara (business Plan) kati ya Vijana **30** walioshiriki mashindano hayo.

v. Vijana **20** (wanawake 10 na wanaume 10) wamepatiwa mafunzo ya ujuzi katika fani ya ushoni, upishi na ufundi wa Aluminum pamoja na kupatiwa vitendea kazi vyenye thamani ya **Shilingi 100,000,000** kwa ufadhili wa Shirika linaloshughulikia Afya ya Jamii na Ustawi Afrika (COMHESWA) ili waweze kutumia ujuzi waliopata na vifaa hivyo kuweza kujiajiri.

vi. Madereva **1,563** (1,164 Unguja na 399 Pemba) waliomba ajira ya udereva **nchini Qatar** kati ya hao **927** (796 Unguja na 131 Pemba) walifanyiwa usaili. Madereva **501** sawa na asilimia **54** (475 Unguja na 26 Pemba) walifaulu kati ya hao **107** (93 Unguja na 14 Pemba) watasafiri kwa awamu ya kwanza kwenda kufanyakazi katika Kampuni ya MOWASALAT.

vii. Madereva **200** (Unguja 130 na 70 Pemba) ambao hawakufaulu kwenye usaili wa ajira ya udereva za Qatar, walipatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa lugha ya Kiengereza na kuimarisha tabia njema ili kukidhi vigezo vya fursa za ajira.

viii. Watendaji **8** kutoka Kampuni za Mawakala wa Ajira Binafsi wamepatiwa mafunzo ya Usafirishaji wa watafuta Ajira unaozingatia maadili (*Ethical Recruitment*) kwa kushirikiana na Shirika linaloshughulikia Wafanyakazi wahamaji Dunani -IOM.

**PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI NA UIMARISHAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA**

**34. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inajukumu la kufanya usajili, usimamizi, ukaguzi na uimarishaji wa Vyama vya Ushirika.

**35. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika, ilitengewa **Shilingi 721,443,000** kati ya hizo **Shilingi 306,243,000** mshahara na **Shilingi 415,200,000** kwa matumizi ya kawaida.

**36. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, **Shilingi 534,091,753** kati ya hizo **Shilingi 229,682,250** mshahara na shilingi **304,409,503** matumizi ya kawaida zilikadiriwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, Programu hii, imeingiziwa **Shilingi 333,476,573** sawa na asilimia **62** kati ya hizo **202,731,925** sawa na asilimia **88** mshahara na **Shilingi 130,744,648** sawa na asilimia **43** matumizi ya kawaida.

37. **Mheshimiwa Spika,** Shughuli zilizotekelezwa na programu hii ni kama zifuatavyo:-

i. Wizara imesajili Vyama vya Ushirika **1,071** (Unguja 660 na Pemba 411) na kufanya Ukaguzi wa hesabu za Vyama vya Ushirika **210** (Unguja 111 na Pemba 99) pamoja na kufanya Ufuatiliaji wa Vyama vya Ushirika **814** (Unguja 616 na Pemba 198). **Kiambatisho namba 3 kinafafanua.**

ii. Wanachama wa vyama vya ushirika **5,547** (4,120 Wanawake na 1,427 Wanaume) kutoka Vyama vya Ushirika **954** (685 Unguja na 269 Pemba) wamepatiwa mafunzo ya Dhana ya Ushirika, Mabadiliko ya Mtazamo, Uandishi wa Ripoti, Uwekaji wa Kumbukumbu za hesabu, Uongozi na Utawala Bora. Aidha, Watendaji **16** (Wanawake 8 wa 8 Wanaume) wa SACCOS walipatiwa taaluma fupi juu ya uandishi wa Mpango wa Biashara na taarifa za kifedha.

iii. Wizara kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kutoa mafunzo ya Kanuni mpya za Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) na Usimamizi wa Fedha kwa Viongozi **207** wa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo **39**.

iv. Wizara kwa Mashirikiano na Chama cha Mazingira na Ufugaji Tija Tanzania (CHAMAUTA) imeibuwa Progamu ya "Vijana Tujenge Ajira Pamoja" (VITAP), inatarajiwa kuzalisha ajira **50,000** kufikia mwaka 2030. Kwa

awamu ya kwanza, Programu hiyo itagawa vifaranga **500** kati ya **3,000** vilivyopangwa kupewa Vijana kupitia Mradi huu.

v. Wizara imeadhimisha siku ya Ushirika Duniani ambapo kilele chake kilifanyika tarehe 5 Julai 2025 katika Viwanja vya Kizimkazi Dimbani Mkoa wa Kusini Unguja. Kauli mbiu ya Siku ya Ushirika ilikua "***Ushirika Hujenga Ulimwengu Bora"***. Maadhimisho hayo yaliambatana na shughuli za Usafi katika maeneo ya Bandari ya Malindi na Funguni.

vi. Wizara iliandaa kongamano la uhamasishaji wa Vijana kujiunga na Vyama vya Ushirika. Kongamano hilo lilifanyika katika Vyuo vya Amali (VTA) vya Mwanakwerekwe, Makunduchi na Mkokotoni na kuwashirikisha Wataalamu na Wadau wa Ushirika. Vijana **167** (wanawake 60 na Wanaume 107) walishiriki. Kauli mbiu ya kongamano hilo ilikuwa ni ***"Ushirika ni Biashara".***

vii. Wizara imehamasisha Vyama vya Ushirika kununua hisa kwenye Benki ya Ushirika Tanzania. Katika utekelezaji wa hilo Chama cha Ushirika cha Wachukuzi Bandarini (Beach Porter) kimeweza kununua hisa zenye thamani ya **Shilingi 2,000,000** na kupatiwa hati ya umiliki wa hisa. Aidha, baada ya mwaka mmoja wataweza kupatiwa faida ya uwekezaji wa hisa.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA

38. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imeanza mara baada ya kuundwa kwa Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji mwezi Novemba 2025 na imepangiwa fedha kutoka **Fungu A07** - Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji na **Fungu J03** - Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa lengo la kufanikisha shughuli za Uendeshaji na Uratibu wa Wizara kwa Unguja na Pemba. Aidha fedha hizo zimepangwa kutumika kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2026.

39. **Mheshimiwa Spika,** Progamu hii ina lengo la kuhakikisha kuwa Wizara inatayarisha na kuratibu utekelezaji wa mipango, Sera na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Programu hii ina Programu ndogo tatu ambazo ni Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara na Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba.

## PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI

40. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inajukumu la Uendeshaji na Uimarishaji wa nguvu kazi katika Wizara.

41. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jumla ya wafanyakazi **130** wakiwemo wafanyakazi 73 waliotoka katika Idara zilizounganishwa na Wizara na wafanyakazi 57 waliopokelewa kutoka taasisi mbali mbali kupitia Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa njia ya Uhamisho wa Kuazimwa.

42. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha shughuli za Uendeshaji na Uratibu wa Wizara **Shilingi 577,055,000** zimepangwa kutumika kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2026. Hadi kufikia Machi, 2026 Shilingi **385,500,000** sawa na asilimia **67** zilipatikana kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

43. **Mheshimiwa Spika,** Shughuli zilizotekelezwa na programu hii ni kama zifuatavyo:-

i. Wafanyakazi **73** (46 Unguja na 27 Pemba) wakiwemo wanawake 36 na wanaume 37 wamefanyiwa mafunzo ya ndani ya Sheria **Namb. 2** ya mwaka 2011 na Kanuni za utumishi wa Umma ya Mwaka 2014. Aidha, Wizara imetoa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa e-Office kwa watendaji.

ii. Wafanyakazi **14** (Wanawake 9 na Wanaume 5) wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya muda mfupi **8** na mrefu **6** katika fani za TEHAMA, Ukatibu Mahsusi, mahusiano kazini, Ustawi wa Jamii, Upangaji wa Miradi na Udereva.

iii. Watendaji **10** wa Wizara wamepatiwa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Takwimu (STATA) kwa mashirikiano na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia Mradi wa Kuimarisha Taaluma za Ajira kwa Vijana inayoendana na Soko la Uchumi wa Bluu (SEBEP) katika Chuo cha Takwimu cha Afrika Mashariki (EASTC)-Dar es Salaam.

iii. Wizara imeendelea kulipa stahiki za wafanyakazi zikiwemo malipo baada ya saa za kazi kwa wafanyakazi sita (6), likizo kwa wafanyakazi wawili (2), malipo ya safari za kikazi kwa wafanyakazi (14), kuwalipa fedha za Ubani wafanyakazi wawili (2) na maposho mbali mbali.

iv. Wizara imeratibu safari za kikazi kwa Viongozi na Watendaji ikiwemo Unguja, Pemba na Tanzania Bara. Aidha, Wizara imefanya malipo ya huduma za Uendeshaji ikiwemo; ulinzi, usafi na umeme.

v. Wizara imefanikiwa kuimarisha mazingira ya wafanyakazi kwa kukodi jengo na kuingiza samani za Ofisi katika eneo la Magomeni Wandaras na Gombani kwa Upande wa Pemba.

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA TAFITI ZA WIZARA**

**44. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inajukumu la kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mipango, sera na tafiti za Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji**.**

**45. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha shughuli za Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti Programu hii imepangiwa **Shilingi 132,196,000** kwa kipindi Januari hadi Juni 2026. Hadi kufikia Machi, 2026, **Shilingi 44,500,000** sawa na asilimia **34** zilipatikana kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

46. **Mheshimiwa Spika,** Shughuli zilizotekelezwa na programu hii ni kama zifuatavyo:-

i. Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanikiwa kuandaa ripoti za utelekezaji kwa kipindi cha miezi mitatu, sita na tisa kwa mwaka fedha wa 2025/2026. Sambamba na hilo, Idara imeratibu uandaaji wa Taarifa za Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi pamoja Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

ii. Wizara inaendelea na matayarisho ya kuandaa Mpango Mkakati wa miaka mitano 2025–2030 wa Sekta ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji, kwa sasa upo katika hatua ya ukusanyaji wa maoni ya Wadau kwa ukamilishaji.

iii. Maafisa **30** (20 Unguja na 10 Pemba) wa Wizara wamepatiwa mafunzo ya kuandaa Mpangokazi (MTEF, POA, PBB) wa Mwaka wa fedha 2026/2027.

iv. Wizara imefanikiwa kuandaa rasimu ya Mpango Mkakati wa upatikanaji wa fursa za ajira (2025-2030) kwa Wazawa hasa Vijana. Mkakati huo unalenga Ukuaji wa uchumi, maendeleo ya ujuzi na uhamaji wa ajira kimataifa na umepangwa kutekelezwa katika Wizara, Taasisi na Sekta Binafsi kwa maeneo **saba** ambayo yatazalisha ajira za moja kwa moja **237,000** na ajira zisizokua za moja kwa moja **152,000** kufika ajira **389,000** ifikapo 2030. **Kiambatisho namb. 4** Kinafafanua zaidi.

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA**

47. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya uratibu na kusimamia Utawala, Uendeshaji wa Ofisi kuu Pemba inajukumu la kuratibu shughuli zote za Wizara Pemba ikiwemo Uendeshaji, Uimarishaji wa nguvu kazi na uratibu wa mipango.

48. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha shughuli za Uendeshaji na uratibu wa Wizara Pemba **Shilingi 211,000,000** zimepangwa kutumika kwa kipindi Januari hadi Juni 2026. Hadi kufikia Machi, 2026 **Shilingi 52,920,000** sawa na asilimia **25** zilipatikana kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

49. **Mheshimiwa Spika,** Shughuli zilizotekelezwa na Programu hii ni kama zifuatavyo:-

    i. Ofisi Kuu Pemba imeweza kuimarisha mazingira mazuri ya kazi kwa kuwapatia Wafanyakazi Samani, vifaa vya Ofisi na vya kuandikia ili kuimarisha mazingira mazuri kwa Watendaji.

    ii. Ofisi kuu Pemba imeendelea kulipa stahiki muhimu za wafanyakazi zikiwemo malipo baada ya saa za kazi kwa wafanyakazi watatu **(3),** likizo kwa wafanyakazi wawili **(2)** pamoja na malipo ya safari kikazi kwa wafanyakazi sita **(6)**.

iii. Wafanyakazi **27** (wanawake 10 na wanaume 17) wamepatiwa mafunzo ya sheria, kanuni na miongozo ya kiutumishi. Aidha ofisi imefanikiwa kufanya vikao **(3)** vya utendaji kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

iv. Ofisi imefanya matengenezo madogo madogo katika jengo la Ofisi Kuu Gombani.

**WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

**50. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imetekeleza Programu kuu mbili ambazo ni:-

i. Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

ii. Programu ya Uendeshaji na Utumishi wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

**UPATIKANAJI WA FEDHA**

**51. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar ilikadiriwa kutumia **Shilingi 14,656,600,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,056,600,000** (2,323,200,000 kwa matumizi mengineyo na Shilingi 1,733,400,000 kwa mshahara) na **Shilingi 10,600,000,000** kwa shughuli za maendeleo.

52. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar, ilikadiriwa kutumia **Shilingi 11,203,508,250.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 3,253,508,250** (1,953,458,250 kwa matumizi mengineyo na Shilingi 1,300,050,000 kwa mshahara) na **Shilingi 7,950,000,000** kwa shughuli za maendeleo.

53. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2026 Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar imeingiziwa **Shilingi 7,801,293,672** sawa na asilimia **70.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 646,892,505** sawa na asilimia **33** kwa matumizi mengineyo, **Shilingi 1,851,814,500.50** sawa na asilimia **142** mshahara na **Shilingi 5,302,586,667** sawa na asilimia **67** kazi za maendeleo. **Kiambatisho 5A, 5B,** na **5C** kinafafanua.

## UTEKELEZAJI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

## PROGRAMU KUU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

54. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kuwawezesha Wananchi Kiuchumi kwa kuwapatia mafunzo, mikopo na kuwaunganisha na fursa za masoko na inatekelezwa na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar. Programu hii ina Programu ndogo moja ya Uwezeshaji Wananchi kiuchumi.

55. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uwezeshaji Wananchi kiuchumi, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ilitengewa jumla ya **Shilingi 11,064,500,000** kati ya hizo **Shilingi 464,500,000** matumizi ya kawaida na **Shilingi 10,600,000,000** kwa Mradi wa maendeleo.

56. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, **Shilingi 8,337,633,000** zilikadiriwa kutumika kati ya hizo, **Shilingi 387,633,000** matumizi ya kawaida na **Shilingi 7,950,000,000** mradi wa maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, Programu hii imeingiziwa **Shilingi 5,404,044,992** sawa na asilimia **65.** Kati ya hizo **Shilingi 101,458,325** matumizi ya kawaida sawa na asilimia **26** na **shilingi 5,302,586,667** sawa na asilimia **67** mradi wa maendeleo.

57. **Mheshimiwa Spika,** Shughuli zilizotekelezwa na programu hii ni kama zifuatavyo:-

    i. Kamati **11** (Unguja 7 na Pemba 4) za uratibu wa mikopo ya makundi maalumu (4.4.2) kutoka Serikali za Mitaa zimepatiwa taaluma ya mikopo na matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Mikopo. Aidha, imekutana na Masheha wa Wilaya; Kati, Magharibi “A”, Kaskazini “A” Kaskazini “B” na Mjini kwa Unguja na Wilaya zote kwa Pemba kuzungumzia taratibu za mikopo na hali halisi ilivyo pamoja na mikakati mengine ya kusimamia masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika maeneo yao.

ii. **Shilingi 508,999,106.42** sawa na asilimia **10** ya mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepokelewa kwa lengo la kutoa mkopo kupitia Programu ya Makundi Maalumu ya Wajasiriamali, Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu**. Kiambatanisho namb 6A** kinafafanua.

iii. **Shilingi 12,779,637,967** (Unguja Shilingi 11,198,327,704 na Pemba Shilingi 1,581,310,263) zimetolewa mikopo kwa Wananchi **6,135** (Unguja 5,543 na Pemba 592)**. Kiambatanisho namb 6B** kinafafanua.

iv. **Shilingi 5,668,172,841.49** (Unguja Shilingi 4,562,257,942.64 na Pemba Shilingi 1,105,914,898.85) za marejesho ya mikopo zimekusanywa sawa na asilimia **18** ya matarajio. **Kiambatanisho namb 6C** kinafafanua.

v. Wajasiriamali **2,609** walipatiwa mafunzo, kati ya hao Unguja **1,234** (wanaume 343 na wanawake 891) na Pemba **1,375** (wanaume 397 na wanawake 978). Mafunzo hayo ni elimu ya fedha, usarifu wa matunda na mbogamboga na upambaji wa uso (make up) na mengineyo**. Kiambatanisho namb 6D** kinafafanua.

vi. Wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati (MSMEs) **26** (Unguja 21 na Pemba 5) wamesaidiwa kukuza Teknolojia kwa kufanya matengenezo ya mashine 4 za uzalishaji pamoja na kupatiwa ushauri wa kitaalamu wa uzalishaji.

vii. Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar imefanya matengenezo ya mashine 7 katika Kituo cha Kukuza na Kulea Wajasiriamali Pemba ili kuongeza ufanisi.

viii. Wajasiriamali **101** (wanaume 30 na wanawake 71) na Kampuni **50** za Wajasiriamali wameunganishwa na fursa za masoko kwa kupitia maonesho mbali mbali, sawa na asilimia **39** ya lengo la wajasiriamali **392** kwa mwaka.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA UTUMISHI YA WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

**58. Mheshimiwa Spika,** Progamu hii ina lengo la kuhakikisha kuwa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inatayarisha mipango na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Programu hii ina Programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji, na Programu ndogo ya Afisi ya Uratibu wa shughuli za Wakala Pemba.

## PROGRAMU NDOGO YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

**59. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inajukumu la Uendeshaji na Uimarishaji wa nguvu kazi katika Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, kuratibu na kusimamia ufuatiliaji na utekelezaji wa mipango ya Taasisi.

**60. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ilitengewa jumla ya **Shilingi 2,881,166,000** kati ya hizo **Shilingi 1,408,700,000** matumizi ya kawaida na **Shilingi 1,472,466,000** Mshahara.

**61. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, **Shilingi 2,303,640,750** zilikadiriwa kutumika kati ya hizo, **Shilingi 1,199,291,250** matumizi ya kawaida na **Shilingi 1,104,349,500** Mshahara. Hadi kufikia Machi 2026, Programu hii imeingiziwa **Shilingi 1,886,927,143** sawa na asilimia 82 Kati ya hizo **Shilingi 414,614,680** matumizi ya kawaida sawa na asilimia **35** na **shilingi 1,472,312,463** sawa na asilimia **133** Mshahara.

**62**. **Mheshimiwa Spika,** Shughuli zilizotekelezwa na programu hii ni kama zifuatavyo:-

i Wafanyakazi **18** (wanaume 12 na wanawake 6) wamejengewa uwezo kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi katika fani za Sheria, Uongozi, ukaguzi, Uhusiano wa Umma, Udereva, na usimamizi wa vihatarishi.

ii Wafanyakazi **76** wamepatiwa mafunzo ya ndani ya usimamizi wa viashiria hatarishi na uzingatiaji wa Siha na Lishe katika mazingira ya kazi.

iii Vikundi **380** (Unguja 256, Pemba 124) vilivyopatiwa mikopo vilifanyiwa ufuatiliaji kwa ajili ya kujua maendeleo na changamoto zao ambavyo ni; Programu ya Nyuki, INUKA, MSME (Khalifa) na Makundi maalumu (4.4.2), sawa na asilimia 95 ya lengo la wajasiriamali/ vikundi 400 kwa mwaka.

iv Vipindi **13 (7** Redio na **6** TV) kupitia ZBC na Spice FM na machapisho **14** yaliandaliwa ya kuelimisha jamii juu ya Uwezeshaji na huduma zinazopatikana Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (ZEEA) yalisambazwa kwa jamii.

**PROGRAMU NDOGO YA AFISI YA URATIBU WA WAKALA PEMBA**

**63. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inajukumu la kuratibu shughuli zote za Wakala Pemba zikiwemo huduma za Uwezeshaji, Uendeshaji, Uimarishaji wa nguvu kazi na uratibu wa mipango.

**64. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ilitengewa jumla ya **Shilingi 710,934,000** kati ya hizo **Shilingi 450,000,000** matumizi ya kawaida na **Shilingi 260,934,000** Mshahara.

**65. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, **Shilingi 562,234,500** zilikadiriwa kutumika kati ya hizo, **Shilingi 366,534,000** matumizi ya kawaida na

**Shilingi 195,700,500** Mshahara. Hadi kufikia Machi 2026, Programu hii imeingiziwa **Shilingi 510,321,538** sawa na asilimia 91 Kati ya hizo **Shilingi 130,819,500** matumizi ya kawaida sawa na asilimia **36** na **shilingi 379,502,038** sawa na asilimia **193** Mshahara.

**66. Mheshimiwa Spika,** Shughuli zilizotekelezwa na programu hii ni kama zifuatavyo:-

i Ofisi ya uratibu Pemba imeweza kuimarisha mazingira mazuri ya kazi kwa kuwapatia Wafanyakazi vitendea kazi, vikiwemo vifaa vya kuandikia. Aidha, imegharamia huduma za uendeshaji zikiwemo huduma za umeme, maji na usafi ili kuimarisha mazingira mazuri kwa Watendaji.

ii Wafanyakazi **5** (Wanaume 4 na mwanamke 1) wamejengewa uwezo kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi katika fani za Uongozi, Udereva, Usimamizi wa fedha, Utunzaji wa kumbukumbu na Uandishi wa habari.

iii Ofisi ya uratibu Pemba imeratibu utoaji wa huduma za uwezeshaji zikiwemo za mikopo na mafunzo, kwa upande wa wananchi waliopo katika Jiografia ya Pemba na kuwasilisha ripoti za utekelezaji katika Afisi kuu Unguja.

## E. CHANGAMOTO NA NJIA ZA UTATUZI

67. **Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara kupitia Idara na Taasisi zake, ilikabiliwa na baadhi ya changamoto zifuatazo;

i. Ukosefu wa ajira kwa vijana, ujuzi na mahitaji ya soko la Ajira;

ii. Vijana kutokidhi vigezo vya mikopo vilivyowekwa na taasisi za kifedha ikiwemo dhamana;

iii. Upatikanaji mdogo wa mitaji na fursa za biashara;

iv. Uratibu mdogo wa wadau wa masuala ya Vijana, Ajira, Ushirika na Uwezeshaji;

v. Matumizi ya dawa za kulevya, Ushawishi wa kundi rika na Matumizi mabaya na yasiyosahihi ya mitandao ya kijamii;

vi. Kuongezeka kwa tatizo la Afya ya Akili na msongo wa mawazo;

vii. Kuchelewa kukamilika kwa mifumo ya kieletroniki katika upatikanaji wa taarifa mbali mbali kutokana na upya wa Wizara;

viii. Uhaba wa Ofisi na vitendeakazi kwa Wizara;

ix. Kuchelewa kwa uingizwaji wa fedha;

x. Uhaba wa vyombo vya usafiri kwa Watendaji; na

xi. Uhaba wa wafanyakazi.

## UTATUZI WA CHANGAMOTO

68. **Mheshimiwa Spika;** Kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji majukumu hayo, Wizara imejipanga kutatua kama ifuatavyo:-

i. Wizara inaendelea kuweka mifumo madhubuti ya Kisera, Sheria, Mikakati na mifumo ya taarifa za soko la ajira ili kufuatilia mwenendo wa mahitaji ya ajira na nguvu kazi pamoja na kulinda ajira za Wazawa. Hatua hii inalenga kusaidia katika kupanga sera na mikakati ya kukuza ajira nchini;

ii. Wizara imeanza kutekeleza utaratibu wa kupunguza masharti na kuweka dirisha maalumu kwa Vijana (soft loan);

iii. Wizara kwa kushirikiana na Taasisi za kifedha imeweka malengo kwa ajili ya kuwapatia mitaji vijana ambao wameanzisha biashara na shughuli za uzalishaji mali;

iv. Wizara imeandaa programu za mafunzo na uhamasishaji juu ya kujenga uzalendo, athari za matumizi ya dawa za kulevya na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii na kuachana na vitendo viovu;

v. Wizara imetenga fedha katika bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya kidijitali;

vi. Wizara imepeleka maombi Serikalini kupatiwa vifaa na limeanza kutekelezwa. Aidha, imekodi jengo la Ofisi ya Wizara Unguja na kutenga bajeti kodi ya jengo mwaka wa fedha 2026/2027;

vii. Wizara inaendelea kuwasiliana na Wizara ya fedha ili iweze kuingizwa fedha kwa wakati; na

viii. Wizara imepanga Bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/ 2027 kwa ajili ya ununuzi wa gari tano.

## F. MUELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**69. Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imezingatia Mipango ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya mwaka 2050, Mpango Mkuu wa Maendeleo Zanzibar 2026-2031, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025-2030, Maagizo ya Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Sera, Sheria, Miongozo na Mpango Mkakati wa Wizara na Malengo ya Dunia ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

**70. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara itaendelea kutekeleza mpango wake kupitia Programu zake Kuu **Tatu** na Programu Ndogo **Saba**.

## VIPAUMBELE VYA WIZARA

71. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara imepanga kutekeleza vipaumbele **nane** vifuatavyo:-

i. Kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya vijana nchini na kuwawezesha vijana kwa kuwajengea uwezo ili kuimarika kiuchumi, kijamii na kisiasa;

ii. Kuimarisha Mabaraza ya Vijana kiutendaji na kuhamasisha ushiriki na ushirikishwaji wa vijana katika fursa mbali mbali kupitia ngazi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;

iii. Kuratibu upatikanaji wa Ajira za staha **70,000** kwa wote kwa kushirikiana na wadau ndani na nje ya nchi;

iv. Kuimarisha maendeleo ya Vyama vya Ushirika nchini;

v. Kuimarisha na kuanzisha mifumo ya kielektroniki yenye kusomana kwa ukusanyaji wa taarifa (Kanzidata);

vi. Kuwawezesha Wananchi 28,339 kiuchumi kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu yenye thamani ya Shilingi Bilioni 47.3**;**

vii. Kuandaa na kufanya mapitio ya Sera, Sheria, kanuni, miongozo na mikakati ya Wizara pamoja na kuimarisha ufanyaji wa tafiti, ufuatiliaji na tathmini; na

viii. Kuimarisha uhusiano na mashirikiano kati ya Wizara, Taasisi, Wadau wa ndani na nje ya nchi.

## G. PROGRAMU ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### PROGRAMU KUU (P01): UENDESHAJI NA URATIBU WIZARA

**72. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina programu ndogo tatu ambazo ni **S0101** - Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti, **S0102** - Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji na **S0103** - Programu ndogo ya Uratibu na Uendeshaji wa shughuli za Wizara Pemba. Programu hii imetengewa **Shilingi 4,802,804,000** kati ya hizo **Shilingi 2,648,072,000** kwa ajili ya mshahara, **Shilingi 2,154,732,000** matumizi mengineyo.

**73. Mheshimiwa Spika**, Programu hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kukamilisha Mpango Mkakati wa Wizara na Kuratibu utekelezaji wa mipango, mikakati na miradi ya maendeleo ya wizara;

ii. Kuandaa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E Framewok) na kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Ushirika na Sera ya Ajira;

iii. Kuimarisha upatikanaji wa takwimu za Wizara na kufanya tafiti za sekta;

iv. Kuimarisha mashirikiano na Wizara, Taasisi na mashirika Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;

v. Kuimarisha utendaji kwa kuwajengea uwezo Wafanyakazi **90** kwa kuwapatia mafunzo ya ndani, muda mfupi na muda mrefu;

vi. Kuimarisha huduma za uendeshaji za Wizara ikiwemo Ununuzi wa Vifaa, malipo na matengenezo ya Ofisi, usafi, usafiri, mawasiliano na ulinzi;

vii. Kuimarisha usafiri kwa viongozi na watendaji kwa kununua magari matano;

viii. Kuendelea kusimamia maslahi na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao zikiwemo za mishahara likizo na stahiki nyengine kwa mujibu wa miongozo ya kiutumishi;

ix. Kuanzisha na kuimarisha mifumo ya Ofisi ikiwemo e-office, Assets Register na HRM;

x. Kuratibu shughuli za Ofisi Kuu Pemba.

**PROGRAMU KUU (P02): MAENDELEO YA VIJANA**

**74. Mheshimiwa Spika,** Programu hii itakuwa na programu ndogo mbili; **S0201** - Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana na **S0202** - Programu ndogo ya Baraza la Vijana Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Programu hii imetengewa **Shilingi 12,363,297,923** kati ya hizo **Shilingi 352,430,000** kwa ajili ya mshahara, **Shilingi 781,715,999** matumizi mengineyo (Shilingi 550,628,89

kutoka serikalini na Shilingi 231,087,100 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo), **Shilingi 10,000,000,000** Miradi ya maendeleo na **Shilingi 1,229,151,924** (Shilingi 221,150,000 Mshahara na Shilingi 1,008,001,924 matumizi mengineyo) ni Ruzuku kwa Baraza la Vijana.

**75. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo;

i. Kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, wiki ya Vijana na Kumbukizi ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius K Nyerere;

ii. Kuimarisha na kuratibu Vituo vya Mafunzo, Taasisi na Vikundi vya Kiuchumi vya Vijana;

iii. Kuratibu maadhimisho ya siku ya Vijana Kimataifa na Kongamano la Kitaifa la Vijana la Miaka 63 ya Mapinduzi ya Zanzibar;

iv. Kuratibu programu za elimu, malezi na makuzi kwa vijana pamoja na mikakati ya kujenga moyo wa Uzalendo, kujitolea na kuipenda nchi yao;

v. Kufanya ufuatiliaji na kuyaimarisha Mabaraza ya vijana katika ngazi ya Shehia, Wilaya na Taifa; na

vi. Kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

## PROGRAMU KUU (P03) URATIBU WA UPATIKANAJI WA AJIRA ZA STAHA KWA WOTE NA MAENDELEO YA USHIRIKA

**76.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina programu ndogo mbili ambazo ni **S0301** - Programu ndogo ya Ajira za Staha kwa wote na **S0302** - Programu ndogo ya Usajili, Usimamizi, Ukaguzi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Programu hii imetengewa jumla ya **Shilingi 1,884,137,000** kati ya hizo **Shilingi 499,498,000** mshahara, **Shilingi 1,384,639,000** matumizi mengineyo (Shilingi 1,234,639,000 kutoka Serikalini na Shilingi 150,000,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**77.** **Mheshimiwa Spika**, Programu hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo;

i. Kufanya utafiti kuhusu mahitaji ya soko la ajira;

ii. Kukamilisha uandaaji wa Sheria ya uundaji na ukuzaji wa Ajira;

iii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera, mipango, programu na mikakati inayohusiana na masuala ya ajira Zanzibar;

iv. Kushiriki katika mikutano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kuhusiana na masuala ya ajira;

v. Kufanya usajili, usimamizi na ukaguzi wa hesabu kwa Vyama vya Ushirika;

vi. Kuimarisha huduma za Ushirika kupitia mafunzo na matokeo ya tafiti;

vii. Kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Ushirika;

viii. Kufanya vikao vya ushirikiano na wadau (Moshi Cooperative University, Tanzania Cooperative Development Commission, Chama cha Mazingira na Ufugaji Tija Tanzania na Benki ya Ushirika Tanzania) ili kusaidia utekelezaji wa afua za ushirika;

ix. Kushughulikia utatuzi wa migogoro ya Vyama vya Ushirika; na

x. Kuratibu Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo.

**WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI Fungu (105)**

**78. Mheshimiwa Spika,** Fungu hili lina Programu kuu mbili ambazo ni Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Programu ya Uendeshaji na Utumishi (P01) na Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (P02).

**79. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar inaomba kuidhinishiwa makadirio ya jumla ya **Shilingi 52,850,532,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,486,340,000** kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 3,064,192,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **TZS 47,300,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**PROGRAMU KUU (P01) UENDESHAJI NA UTUMISHI WA WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

80. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina programu ndogo mbili ambazo ni: -

i. Programu Ndogo ya Utumishi na Uendeshaji
ii. Programu Ndogo ya Ofisi ya Uratibu wa Wakala Pemba.

81. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo;

i. Kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi watendaji **52** (Unguja 40 na Pemba 12) pamoja na kulipa stahiki kwa wafanyakazi kulingana na taratibu za kiutumishi;

ii. Kutayarisha Mifumo ya kidigitali ya ufuatiliaji na Tathmini na ukusanyaji wa taarifa za ndani ya Taasisi;

iii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa wanufaika **400** wa huduma za Uwezeshaji;

iv. Kutayarisha Miongozo ya matumizi ya TEHAMA kwa Taasisi (Sera na Mkakati);

v. Kusaidia Wajasiriamali **300** katika kutumia mifumo ya kidigitali ya utoaji wa huduma za uwezeshaji; na

vi. Kuelimisha jamii kuhusu fursa za Uwezeshaji kupitia vyombo vya Habari, mitandao ya kijamii na mikutano na wananchi.

## PROGRAMU KUU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZANZIBAR (P02)

**82. Mheshimiwa Spika,** Programu hii itakuwa na programu ndogo moja ambayo ni: -

**S0201**- Programu Ndogo ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

**83. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo;

i. Kutoa taaluma kwa masheha wa Unguja na Pemba kwa Halmashauri na Manispaa **11** (Unguja 7 na Pemba 4) kuhusiana na masuala ya uwezeshaji;

ii. Kutoa mikopo yenye masharti nafuu ya thamani ya **Shilingi 47,300,000,000** (Unguja **Shilingi** 30,750,000,000 na Pemba **Shilingi** 16,560,000,000) kwa wananchi **28,339** (Unguja 18,420 na Pemba 9,919);

iii. Kutoa mafunzo ya Uwezeshaji kulingana na mahitaji kwa wananchi **4,300** (Unguja 2,300 na Pemba 2,000);

iv. Kufanya utambuzi kwa wajasiriamali **12** (Unguja 8 na Pemba 4) waliofanikiwa katika sekta tofauti zikiwemo Kilimo, Utalii na Uchumi wa Buluu na kuwatumia kama sehemu za mafunzo ya vitendo kwa Wajasiriamali wengine;

v. Kuwaunganisha wajasiriamali, wazalishaji na wafanyabiashara **392** (Unguja 235 na Pemba 157) na fursa za masoko;

vi. Kutoa msaada wa kitaalamu kwa wajasiriamali wadogo wadogo na wakati (MSMEs) **70** (Unguja 30 na Pemba 40); na

vii. Kuibua ubunifu kwa Vijana **sita** na kuwaendeleza kwa kuwaunganisha na fursa zinazohitajika.

## H. SHUKRANI

**84. Mheshimiwa Spika**, Nichukue fursa hii sasa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa busara na ustahmilivu mkubwa aliouonesha katika uongozi na usimamizi wa maendeleo ya nchi yetu kwa amani na utulivu. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kusimamia shughuli za Serikali kwa maendeleo ya wananchi wote.

**85. Mheshimiwa Spika,** Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Hassan Khamis Hafidh, Naibu Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi mkubwa. Pia niwashukuru Mawaziri wote kwa ushauri wao na mashirikiano wanayoendelea kunipa katika utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo ya wananchi wetu hasa vijana. Nimshukuru kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Makamu Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa kuendelea kutuongoza na kusimamia vyema mijadala ya Baraza kwa manufaa ya wananchi wote na taifa kwa ujumla.

86. **Mheshimiwa Spika,** kwa nafasi ya kipekee niishukuru Taasisi ya Afisi ya Rais Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji wa Serikali (ZPDB) chini ya Uongozi Mtendaji wake Mkuu Prof. Mohammed Hafidh Khalfan (CEO) kwa mashirikiano wanayoendelea kutupa katika kuhakikisha mpango mkakati wa ajira unatayarisho na kutelelezwa vyema.

87. **Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Makame Mohamed Sufiani Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Uwekezaji na Makamu wake Mheshimiwa Dkt. Mahmoud Omar Hamad, Mheshimiwa Ali Suleiman Mrembo Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bajeti na Wenyeviti wote wa kamati za Baraza la Wawakilishi kwa miongozo yenu mnayotupa katika kufanikisha malengo ya Serikali kwa maendeleo ya Wananchi.

88. **Mheshimiwa Spika,** Niwashukuru kwa dhati wajumbe wako wote wa Baraza hili kwa utulivu na uvumilivu wao kipindi chote nikiwa nawasilisha hutuba ya Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji na naamini michango yao itakuwa chachu ya mafanikio katika utekelezaji wake.

**89. Mheshimiwa Spika,** Niwashukuru watendaji wote wa Wizara kuanzia na Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, Kaimu Afisa Mdhamini Pemba, Wakurugenzi, Katibu Mtendaji Wakala wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, Katibu Mtendaji wa Baraza la Vijana na Watendaji wote wa Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji pamoja na Uongozi wa Mabaraza ya Vijana chini ya Mwenyekiti wake taifa Ndg. Mohamed Abrahman Juma na Makamu wake Ndg.Arishrun Malik Salim na Balozi wa Vijana wa Wizara Mheshimiwa Tawfiq Salim Turky kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha katika uongozi wangu na kuiwezesha Wizara kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kutekeleza majukumu yake.

**90. Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa nikishukuru Chama Changu Cha Mapinduzi, kwa ufuatiliaji mzuri wa Utekelezaji wa Ilani ya Chama tukaweza kufikia asilimia kubwa ya utekelezaji wa maagizo yake na hivyo kupelekea imani kubwa ya Wananchi kwa Chama cha Mapinduzi.

**91. Mheshimiwa Spika,** Sitosahau kuwashukuru wananchi wote wa jimbo langu la Mpendae kwa imani yao kubwa kwangu na mashirikiano wanayonipa katika kuwaletea maendeleo na mimi niendelee kuwaahidi kama sitowatupa. Aidha niishukuru familia yangu kwa ustahamilivu wao mkubwa kwa kipindi chote ambacho sikuwa pamoja nao kwa kunipa utulivu wa kutekeleza majukumu niliyopewa na Serikali.

## I. HITIMISHO

## MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

## A. MAPATO

**92. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako liidhinishe kwa Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji Fungu **055** makusanyo ya Jumla ya **T.Shilingi 100,000,000** ikiwa ni mapato ya Usajili **T.Shilingi 55,000,000** na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika **T.Shilingi 45,000,000**.

## B. MATUMIZI

**93. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, ili Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji iweze kutekeleza Programu kuu na Programu ndogo nilizozieleza, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya **T.Shilingi 19,050,239,024** kwa mchanganuo ufuatao;

- **(i)** **Shilingi 3,500,000,000** kwa ajili ya Mishahara,
- **(ii)** **Shilingi 4,321,087,100** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, kati ya fedha hizo T.Shilingi 3,940,000,000 kutoka Serikalini na T.Shilingi 381,087,100 kutoka kwa Washirika wa Maenedeleo,
- **(iii)** **T.Shilingi 1,229,151,924** Ruzuku kwa Baraza la Vijana na
- **(iv)** **T.Shilingi 10,000,000,000** kwa kutekeleza wa Miradi ya Maendeleo.

**94. Mheshimiwa Spika,** Ili Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Fungu **105** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 iweze kutekeleza mpango kazi wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, naliomba tena Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya **T.Shilingi 52,850,532,000** kwa mchanganuo ufuatao;

**(i)** **T.Shilingi 2,486,340,000** Mishahara**,**

**(ii)** **T.Shilingi 3,064,192,000** Matumizi Mengineyo

**(iii)** **T.Shilingi 47,300,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

***Kiambatisho namb. 7 Kinafafanua.***

**95. Mheshimiwa Spika**, Sasa naliomba Baraza lako lijadili la liidhinishe makadirio ya matumizi ya Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji **T.Shilingi 71,900,771,024**, Kati ya fedha hizo, fungu **055 T.Shilingi 19,050,239,024** na matumizi ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi fungu **105 T.Shilingi 52,850,532,000** kwa mwaka wa fedha 2026/ 2027 ili kuiwezesha Wizara hii kutekeleza majukumu yake.

**96. Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa hoja.

**MHE. SHAABAN ALI OTHMAN (MBM)**
**WAZIRI WA VIJANA AJIRA NA UWEZESHAJI**
**ZANZIBAR.**

# VIAMBATISHO

## *Kiambatisho 1A:* MUHTASARI WA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

| NAMBA YA KASMA | IDARA | CHANZO CHA MAPATO | ENEO | BAJETI YA MWAKA 2025/26 | MAKADIRIO YA MAPATO JULAI -MACHI 2026 | MAPATO HALISI JULAI - MACHI 2026 | ASILIMIA YA MAPATO JULAI - MACHI 2026 | ASILIMIA YA MAPATO MWAKA 2025/26 | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1422075 | AJIRA | UKAGUZI WA UHAKIKI WA MIKATABA YA AJIRA | UNGUJA | 270,000,000 | 204,000,000 | 133,660,000 | 66% | 50% | Upungufu wa wasafiri nje ya nchi |
| | **Jumla ndogo** | | | **270,000,000** | **204,000,000** | **133,660,000** | **66%** | **50%** | |
| 1422036 | MAENDELEO YA USHIRIKA | ADA YA USAJILI | UNGUJA | 160,000,000 | 127,200,000 | 22,680,000 | 18% | 14% | Upungufu unatokana na Uhitaji wa Wananchi |
| 1422037 | | ADA YA UKAGUZI | UNGUJA | 120,000,000 | 88,450,000 | 16,065,000 | 18% | 13% | Upungufu unatokana na uhaba wa wafanyakazi |
| | **Jumla ndogo** | | | **280,000,000** | **215,650,000** | **38,745,000** | **18%** | **14%** | |
| | **Jumla kuu ya Unguja** | | | **550,000,000** | **419,650,000** | **172,405,000** | **41%** | **31%** | |
| 1422036 | MAENDELEO YA USHIRIKA | ADA YA USAJILI | PEMBA | 55,000,000 | 40,300,000 | 12,343,000 | 31% | 22% | Upungufu unatokana na Uhitaji wa Wananchi |
| 1422037 | | ADA YA UKAGUZI | PEMBA | 42,000,000 | 32,100,000 | 2,890,000 | 9% | 7% | Upungufu unatokana na uhaba wa wafanyakazi |
| | **Jumla Kuu ya Pemba** | | | **97,000,000** | **72,400,000** | **15,233,000** | **21%** | **16%** | |
| | **JUMLA KUU YA MAPATO** | | | **647,000,000** | **492,050,000** | **187,638,000** | **38%** | **29%** | |

## *Kiambatisho 1B:* MUHTASARI WA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 (FUNGU 055)

| PROGRAMU | BAJETI YA MWAKA 2025/2026 | MAKADIRIO YA JULAI HADI MACHI, 2026 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI 2025 - MARCH 2026 | ASILIMIA KUANZIA JULAI HADI MACHI, 2026 | ASILIMIA KWA MWAKA 2025/ 2026 |
|---|---|---|---|---|---|
| **P05501: Ajira za Staha** | **1,238,355,000** | **865,009,753** | **637,251,923** | **74%** | **51%** |
| S0550101 Maendeleo ya Ushirika | 721,443,000 | 534,091,753 | 333,476,573 | 62% | 46% |
| S0550102 Ajira za Staha | 516,912,000 | 330,918,000 | 303,775,350 | 92% | 59% |
| **P05502: Uendeshaji na Uratibu** | **920,251,000** | **640,750,000** | **482,920,000** | **75%** | **52%** |
| S055002 Utumishi na Uendeshaji. | 577,055,000 | 395,000,000 | 385,500,000 | 98% | 67% |
| S055001 Mipango, Sera na Utafiti | 132,196,000 | 87,500,000 | 44,500,000 | 51% | 34% |
| S055003 Ofisi kuu Pemba. | 211,000,000 | 158,250,000 | 52,920,000 | 33% | 25% |
| **P05503: Maendeleo ya Vijana** | **18,260,502,690** | **13,823,879,691** | **3,454,968,252** | **25%** | **19%** |
| S055541 Maendeleo ya Vijana | 17,606,041,580 | 13,333,258,858 | 3,044,818,256 | 23% | 17% |
| S055542 Baraza la Vijana | 654,461,110 | 490,620,833 | 410,149,996 | 84% | 63% |
| **JUMLA KUU** | **20,419,108,690** | **15,329,639,444** | **4,575,140,175** | **30%** | **22%** |

## *Kiambatisho 1C:* MMUHTASARI WA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 (FUNGU 055)

| MAELEZO | BAJETI YA MWAKA 2025/2026 | JUMLA YA MAKADIRIO YA JULAI HADI MACHI, 2026 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI 2025 - MARCH 2026 - MSHAHARA | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI -MARCH 2026 - OC | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI -MARCH 2026 MAENDELEO | JUMLA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI-MARCH 2026 | % JULAI - MACHI, 2026 | % MWAKA 2025/ 2026 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **P05501: Ajira za Staha** | **1,238,355,000** | **865,009,753** | **369,111,775** | **268,140,148** | **0** | **637,251,923** | **74%** | **51%** |
| S0550101 Ushirika | 721,443,000 | 534,091,753 | 202,731,925 | 130,744,648 | 0 | 333,476,573 | 62% | 46% |
| S0550102 Ajiraza Staha | 516,912,000 | 330,918,000 | 166,379,850 | 137,395,500 | 0 | 303,775,350 | 92% | 59% |
| **P05502: Uendeshaji na Uratibu** | **920,251,000** | **640,750,000** | **0** | **482,920,000** | **0** | **482,920,000** | **75%** | **52%** |
| S055002 Utumishi na Uendeshaji | 577,055,000 | 395,000,000 | 0 | 385,500,000 | 0 | 385,500,000 | 98% | 67% |
| S055001 Uratibu wa Mipango na Utafiti | 132,196,000 | 87,500,000 | 0 | 44,500,000 | 0 | 44,500,000 | 51% | 34% |
| S055003 Ofisi kuu Pemba | 211,000,000 | 158,250,000 | 0 | 52,920,000 | 0 | 52,920,000 | 33% | 25% |
| **P05503: Vijana** | **18,260,502,690** | **13,823,879,691** | **385,515,672** | **877,063,280** | **2,192,389,300** | **3,454,968,252** | **25%** | **19%** |
| S055541 Vijana | 17,606,041,580 | 13,333,258,858 | 229,432,116 | 622,996,840 | 2,192,389,300 | 3,044,818,256 | 23% | 17% |
| S055542 Baraza la Vijana | 654,461,110 | 490,620,833 | 156,083,556 | 254,066,440 | 0 | 410,149,996 | 84% | 63% |
| **JUMLA KUU** | **20,419,108,690** | **15,329,639,444** | **754,627,447** | **1,628,123,428** | **2,192,389,300** | **4,575,140,175** | **30%** | **22%** |

## *Kiambatisho 2A:* IDADI YA VIJANA WALIOPATIWA MAFUNZO KWA MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2026

| MAELEZO | | UNGUJA | | | PEMBA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S/N | AINA YA MAFUNZO | W'KE | W'ME | TAASISI WALIZOTEKELEZA | W'KE | W'ME | TAASISI WALIZOTEKELEZA |
| 1 | Afya ya uzazi | 5,950 | 4,703 | Idara ya Maendeleo ya Vijana, ZAFAYCO, JUVIEKA, IRCH, YFS, ZAC, PIRO, MIMA,ZAYSO | 3,707 | 3,600 | Idara ya Maendeleo ya Vijana, ZAYCO, SOS, PIRO, UMATI |
| 2 | Stadi za Maisha | 6,238 | 5,847 | Idara ya Maendeleo ya Vijana, JUVIEKA, SAZANI, PYI, ZAFAYCO, CYD, ZADEYO, PIRO, RED CROSS, ZYF, ZAHLAA, ZAYSO. | 4,473 | 3,357 | Idara ya Maendeleo ya Vijana, UVIMAWE |
| 3 | Uongozi na uzalendo | 4,940 | 4,802 | Idara ya Maendeleo ya Vijana, JUVIEKA, CYD, Zanchange Makers, ZAFAYCO, ZAHLIFE, Scouts, MYDO, Zanzibar Youth Council, UVCCM | 7,663 | 4,452 | JUVIEKA, CYD, Zanchange Makers, ZAFAYCO, ZAHLIFE, Scouts, MYDO, Youth Council, UVCCM. |
| 4 | Ushiriki na ushirikishwaji | 6,785 | 5,651 | Idara ya Maendeleo ya Vijana, JUVIEKA, RED CROSS, CYD, Youth Council, ZAHLIFE, Youth with Disability Council, ZAYOVIO, SCOUT, ZAYSO, | 8,947 | 3,933 | Idara ya Maendeleo ya Vijana, PIRO, CYD, SOS, ACTION AIDS, UVIMAWE, NGENARECO, ZAYCO, WACDES |
| 5 | Ujasiriamali na uwezeshwaji | 6,543 | 6,349 | Idara ya Maendeleo ya Vijana, Idara ya Ushirika, Idara ya Ajira, VTA, Wizara ya Kilimo, Uchumi wa buluu, Kamisheni ya Utalii, ZAFAYCO, ZACCA, MYDO, PIRO, Nyota, ZAGCO, Foundation, ZAGCO, Yovio, YUNA, SAZANI, YUNA, CYD, YCI, PDS,ZAYOVIO, PDS, TAYI, ZAYSO | 4,471 | 3,617 | Idara ya Maendeleo ya Vijana, UMATI, ZAYCO, WACDES, PIRO, CYD, UVIMAWE, PSG |
| 6 | Mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi | 5,711 | 5,557 | BOTANIC,YESDO, SAZANI, RED CROSS, Youth Council, JUVIEKA, YOVIO, | 7,208 | 6,492 | Idara ya Maendeleo ya Vijana, ZAYCO, SOS, PIRO, UMATI |
| 7 | Teknolijia ya Habari na Mawasiliano | 5,824 | 5,786 | PYI, ZAFAYCO, ZAYOVIO, PIRO, JUVIEKA, Nyota Foundation, PDS | 1,911 | 1,908 | UMATI, ZAYCO, WACDES, PIRO, CYD, UVIMAWE |
| | | **41,991** | **38,695** | | **38,380** | **27,359** | |
| | **JUMLA** | | **80,686** | | | **65,739** | **146,425** |


*Kiambatisho 2B:* **IDADI YA VIONGOZI WALIOCHAGULIWA KWA WILAYA NA TAIFA**

| WILAYA | WANAWAKE | WANAUME | JUMLA |
|---|---|---|---|
| MJINI | 4 | 8 | 12 |
| MAGHARIBI A | 5 | 7 | 12 |
| MAGHARIBI B | 2 | 10 | 12 |
| KASKAZINI A | 4 | 8 | 12 |
| KASKAZINI B | 7 | 5 | 12 |
| KATI | 4 | 8 | 12 |
| KUSINI | 5 | 7 | 12 |
| WETE | 4 | 8 | 12 |
| MICHEWENI | 4 | 8 | 12 |
| CHAKE-CHAKE | 5 | 7 | 12 |
| MKOANI | 5 | 7 | 12 |
| **JUMLA KWA WILAYA** | **49** | **83** | **132** |
| TAIFA | 2 | 7 | 9 |
| **JUMLA** | **51** | **90** | **141** |

***Kiambatisho 3:*** **IDADI YA VIKUNDI VYA USHIRIKA VILIVYO SAJILIWA, VILIVYOFANYIWA UKAGUZI WA HESABU NA VILIVYOFUATILIWA**

| SN | WILAYA | USAJILI | UKAGUZI WA HESABU | UFUATILIAJI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MJINI | 161 | 26 | 94 |
| 3 | MAGHARIBI A | 99 | 12 | 109 |
| 2 | MAGHARIBI B | 101 | 30 | 91 |
| 4 | KASKAZINI A | 101 | 14 | 62 |
| 5 | KASKAZINI B | 96 | 0 | 67 |
| 7 | KATI | 67 | 25 | 130 |
| 6 | KUSINI | 35 | 4 | 63 |
| 10 | WETE | 120 | 26 | 47 |
| 11 | MICHEWENI | 83 | 28 | 40 |
| 8 | CHAKE-CHAKE | 79 | 18 | 55 |
| 9 | MKOANI | 129 | 27 | 56 |
| **JUMLA** | | **1,071** | **210** | **814** |

*Kiambatisho 4:* **MCHANGO WA KISEKTA KATIKA UIBUAJI WA AJIRA (2026–2030)**



*Kiambatisho 5A:* **UPATIKANAJI WA FEDHA KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2025/2026 (FUNGU 105)**

| Fungu (Vote) | Programu | Makadirio | Kilichopatikana (Total Vote Released) | Matumizi Halisi Julai - Machi 2025/2026 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mshahara | Matumizi Mengineyo | Ruzuku | Maendeleo | Jumla |
| 105 | Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 8,337,633,000 | 5,404,044,992 | 0 | 101,458,325 | 0 | 5,302,586,667 | 5,404,044,992 |
| | Utumishi na Uendeshaji | 2,303,640,750 | 1,886,927,143 | 1,472,312,463 | 414,614,680 | 0 | 0 | 1,886,927,143 |
| | Afisi ya Uratibu - Pemba | 562,234,500 | 510,321,538 | 379,502,038 | 130,819,500 | 0 | 0 | 510,321,538 |
| | **JUMLA** | **11,203,508,250** | **7,801,293,673** | **1,851,814,501** | **646,892,505** | **0** | **5,302,586,667** | **7,801,293,673** |

**_Kiambatisho 5B:_ UPATIKANAJI WA FEDHA KWA PROGRAMU KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2025/2026 (FUNGU 105)**

| PROGRAMU | MAKADIRIO | | | | | MATUMIZI | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | BAGETI YA MWAKA 2025/2026 | MAKADIRIO MISHAHARA MIEZI TISA (JULAI 2025 - MACHI, 2026) | MAKADIRIO OC MIEZI MIEZI TISA (JULAI 2025 - MACHI, 2026) | MAKADIRIO DEVELOPMENT MIEZI TISA (JULAI 2025 - MACHI, 2026) | JUMLA YA MAKADIRIO MIEZI MIEZI MIEZI TISA (JULAI 2025 - MACHI, 2026) | MATUMIZI MISHAHARA MIEZI TISA (JULAI 2025 - MACHI, 2026) | MATUMIZI OC MIEZI MIEZI TISA (JULAI 2025 - MACHI, 2026) | MATUMIZI DEVELOPMENT MIEZI MIEZI TISA (JULAI 2025 - MACHI, 2026) | JUMLA YA MATUMIZI MIEZI MIEZI TISA (JULAI 2025 - MACHI, 2026) | %YA MATUMIZI MIEZI 9 |
| **Program kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi** | **11,064,500,000** | **0** | **387,633,000** | **7,950,000,000** | **8,337,633,000** | **0** | **101,458,325** | **5,302,586,667** | **5,404,044,992** | **65%** |
| Programu ndogo ya Uwezesha Wananchi Kiuchumi | 11,064,500,000 | 0 | 387,633,000 | 7,950,000,000 | **8,337,633,000** | 0 | 101,458,325 | 5,302,586,667 | **5,404,044,992** | 65% |
| **Programu Kuu ya Uendeshaji na Utumishi wa Taasisi ya ZEEA** | **3,592,100,000** | **1,300,050,000** | **1,565,825,250** | **0** | **2,865,875,250** | **1,851,814,501** | **545,434,180** | **0** | **2,397,248,681** | **84%** |
| Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji | 2,881,166,000 | 1,104,349,500 | 1,199,291,250 | 0 | **2,303,640,750** | 1,472,312,463 | 414,614,680 | 0 | **1,886,927,143** | 82% |
| Programu ndogo ya Afisi ya Uratibu - Pemba | 710,934,000 | 195,700,500 | 366,534,000 | 0 | **562,234,500** | 379,502,038 | 130,819,500 | 0 | **510,321,538** | 91% |
| **JUMLA KUU** | **14,656,600,000** | **1,300,050,000** | **1,953,458,250** | **7,950,000,000** | **11,203,508,250** | **1,851,814,501** | **646,892,505** | **5,302,586,667** | **7,801,293,673** | **70%** |

***Kiambatisho 5C:*** **UPATIKANAJI WA FEDHA KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2025/2026 (FUNGU 105)**

| MAELEZO | BAJETI 2025/2026 | MAKADIRIO JULAI - MACHI 2025/2026 | KILICHOPATIKANA (JULAI - MACHI 2025/2026) | ASILIMIA KWA MIEZI 9 (JULAI - MACHI 2025/2026) | ASILIMIA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|
| MISHAHARA | 1,733,400,000 | 1,300,050,000 | 1,851,814,501 | 142% | 107% |
| MATUMIZI MENGINEYO (OC) | 2,323,200,000 | 1,953,458,250 | 646,892,505 | 33% | 28% |
| MIRADI YA MAENDELEO | 10,600,000,000 | 7,950,000,000 | 5,302,586,667 | 67% | 50% |
| **TOTAL** | **14,656,600,000** | **11,203,508,250** | **7,801,293,673** | **70%** | **53%** |

*Kiambatisho 6A:* **MAKUSANYO YA FEDHA KUTOKA HALMASHAURI (UNGUJA NA PEMBA)**

| HALMASAHAURI | FEDHA ILIYOPOKELEWA |
|---|---|
| Baraza la Manispaa Mjini | 30,000,000.00 |
| Baraza la Manispaa Magharibi "A" | 70,990,821.00 |
| Baraza la Manispaa Magharibi "B" | 40,000,000.00 |
| Baraza la Mji Kati | 111,810,991.60 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Kusini | 72,056,859.05 |
| Baraza la Mji Kaskazini "A" | 0 |
| Baraza la Mji Kaskazini "B" | 48,863,415.50 |
| **JUMLA UNGUJA** | **373,722,087.15** |
| Baraza la Mji Chake Chake | 52,172,318.00 |
| Baraza la Mji Mkoani | 31,396,717.26 |
| Baraza la Mji Wete | 29,197,888.65 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | 22,510,095.36 |
| **JUMLA PEMBA** | **135,277,019.27** |
| **JUMLA KUU** | **508,999,106.42** |

***Kiambatisho 6B:*** **UTOAJI WA MIKOPO KUPITIA PROGRAMU ZILIZOPO**

| S/N | PROGRAMU | IDADI YA MIKOPO | THAMANI YA FEDHA | WALIOPATIWA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | W'ME | W'KE | JUMLA |
| | **UNGUJA** | | | | | |
| 1 | INUKA | 491 | 5,994,752,704 | 303 | 401 | 704 |
| 2 | Mikopo ya makundi maalum (4.4.2) | 64 | 530,800,000 | 47 | 645 | 692 |
| 3 | Khalifa/ Abudhabi Fund | 27 | 2,728,275,000 | 75 | 31 | 106 |
| 4 | Dr.Mwinyi Boosting Fund | 3,883 | 1,944,500,000 | 0 | 4,041 | 4,041 |
| | **Jumla Unguja** | **4,465** | **11,198,327,704** | **425** | **5,118** | **5,543** |
| | **PEMBA** | | | | | |
| 1 | INUKA | 134 | 837,310,263 | 125 | 44 | 169 |
| 2 | Mikopo ya makundi maalum (4.4.2) | 89 | 356,000,000 | 25 | 356 | 381 |
| 3 | Khalifa/ Abudhabi Fund | 42 | 388,000,000 | 42 | 0 | 42 |
| | **Jumla Pemba** | **265** | **1,581,310,263** | **192** | **400** | **592** |
| | **JUMLA KUU** | **4,730** | **12,779,637,967** | **617** | **5,518** | **6,135** |

*Kiambatisho 6C:* **MAREJESHO YA MIKOPO**

| S/N | PROGRAMU | UNGUJA | PEMBA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | INUKA | 3,706,104,189 | 1,048,137,452 | 4,754,241,640 |
| 2 | MAKUNDI MAALUM (4:4:2) | 306,965,215 | 34,994,447 | 341,959,662 |
| 3 | KHALIFA | 521,226,039 | 11,000,000 | 532,226,039 |
| 4 | DR. MWINYI BOOSTING FUND (MBF) | 0 | 0 | 0 |
| 5 | MBOGAMBOGA | 3,250,000 | 5,109,000 | 8,359,000 |
| 6 | UWEZESHAJI | 6,740,000 | 6,604,000 | 13,344,000 |
| 7 | SMIDIF | 5,780,000 | 0 | 5,780,000 |
| 8 | VIFAA VYA NYUKI | 12,192,500 | 70,000 | 12,262,500 |
| | **JUMLA KUU** | **4,562,257,943** | **1,105,914,899** | **5,668,172,841** |

*Kiambatisho 6D:* **MAFUNZO KWA WAJASIRIAMALI**

| AINA YA MAFUNZO | W'ME | W'KE | JUMLA |
|---|---|---|---|
| **UNGUJA** | | | |
| Nadharia ya ujasiriamali | 73 | 247 | 320 |
| Usarifu wa matunda na mboga mboga | 0 | 21 | 21 |
| Ufugaji nyuki | 20 | 38 | 58 |
| Elimu ya fedha na usimamizi wa biashara (ikiwemo pre loan) | 196 | 371 | 567 |
| Utengenezaji wa vifaa vya umeme wa jua | 0 | 8 | 8 |
| Utengenezaji wa Sabuni na bidhaa za urembo | 0 | 65 | 65 |
| Utengenezaji wa viungo (spices) | 22 | 6 | 28 |
| Upambaji wa uso (Make Up) | 0 | 52 | 52 |
| Utafutaji wa fursa za masoko na elimu ya fedha | 5 | 12 | 17 |
| Ujasiriamali, masoko, teknolojia na elimu ya fedha | 27 | 51 | 78 |
| Ujasiriamali, Masoko na fursa za ZEEA | 0 | 20 | 20 |
| **Jumla Unguja** | **343** | **891** | **1,234** |
| **PEMBA** | | | |
| Nadharia ya Ujasiriamali | 7 | 53 | 60 |
| Usimamizi wa fedha (Pre-loan) | 272 | 767 | 1,039 |
| Taaluma ya kujisajili na mifumo ya tenda serikalini | 21 | 22 | 43 |
| Uimarishaji wa bidhaa za vipodozi | 8 | 15 | 23 |
| Ushonaji | 0 | 26 | 26 |
| Kilimo cha mboga mboga na matunda | 23 | 15 | 38 |
| Mafunzo ya Upambaji wa uso (Make Up) | - | 50 | 50 |
| Ufugaji wa Nyuki na Uongozi | 37 | 29 | 66 |
| Mabadiliko ya Tabia Nchi | 29 | 1 | 30 |
| **Jumla Pemba** | **397** | **978** | **1,375** |

## *Kiambatisho 7:* MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

| Idara/Taasisi | Mshahara | Matumizi Mengineyo | Ruzuku (Mshahara) | Ruzuku(OC) | Maendeleo | OC Washirika Maendeleo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Utumishi na Uendeshaji** | 1,520,322,000 | 1,358,093,043 | | | | | **2,878,415,043** |
| **Mipango Sera na Utafiti** | 177,750,000 | 400,000,699 | | | | | **577,750,699** |
| **Ofisi Kuu Pemba** | 950,000,000 | 394,147,000 | | | | | **1,344,147,000** |
| | **2,648,072,000** | **2,152,240,742** | | | | | **4,800,312,742** |
| **Ajira** | 222,372,000 | 692,499,140 | | | | 150,000,000 | **1,064,871,140** |
| **Maendeleo ya Ushirika** | 277,126,000 | 427,398,801 | | | | | **704,524,801** |
| | **499,498,000** | **1,119,897,941** | | | | **150,000,000** | **1,769,395,941** |
| **Maendeleo Vijana** | 352,430,000 | 667,861,317 | | | 10,000,000,000 | 231,087,100 | **11,251,378,417** |
| **Baraza la Vijana Zanzibar** | | | 221,150,000 | 1,008,001,924 | | | **1,229,151,924** |
| | **352,430,000** | **667,861,317** | **221,150,000** | **1,008,001,924** | **10,000,000,000** | **231,087,100** | **12,480,530,341** |
| **JUMLA NDOGO KUU** | **3,500,000,000** | **3,940,000,000** | **221,150,000** | **1,008,001,924** | **10,000,000,000** | **381,087,100** | **19,050,239,024** |
| **ZEEA** | | | | | 47,300,000,000 | | **47,300,000,000** |
| **ZEEA** | 2,486,340,000 | 3,020,090,000 | | | | | **5,506,430,000** |
| | **2,486,340,000** | **3,020,090,000** | | | **47,300,000,000** | | **52,806,430,000** |
| | **5,986,340,000** | **6,960,090,000** | **221,150,000** | **1,008,001,924** | **57,300,000,000** | **381,087,100** | **71,856,669,024** |

## Baadhi ya Picha za Matukio mbali mbali yanayoonesha utekelezaji wa Wizara ya Vijana, na Uwezeshaji Zanzibar




***Mhe. Hassan Khamis Hafidh,*** *Naibu Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji akikabidhi hudi ya shilingi 37,200,000 Katika hafla ya uibuaji wa fursa za ujasiriamali kwa Vijana 10 (wanawake 8 na wanaume 2) katika shindano la matayarisho ya mpango wa biashara (business Plan)*



***Mhe. Shaaban Ali Othman****, Waziri wa Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji, akikabidhi vitendeakazi katika Kituo cha Vijana cha Taasisi ya Jendele, Wilaya ya Kati – Mkoa wa Kusini Unguja.*

## Baadhi ya Picha za Matukio mbali mbali yanayoonesha utekelezaji wa Wizara ya Vijana, na Uwezeshaji Zanzibar



***Mhe. Salama Mbarouk Khatib*** *(Kulia) akitia saini hati ya Makubaliano ya Mashirikiano – MoU baina ya Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji na Chama cha Mazingira na Ufugaji Tija Tanzania (CHAMAUTA). Hafla hiyo iliyofanyika Katika Ukumbi wa Chuo cha Utalii Maruhubi.*




***Mhe, Hassan Khamis Hafidh,*** *Naibu Waziri wa Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji akimsaidia kijana mwenye ulemavu kuhudhuria katika mkutano wa kuwashajihisha vijana kushiriki katika uchaguzi wa viongozi, wa Mabaraza ya vijana ngazi ya Shehia, Wilaya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba.*

## Baadhi ya Picha za Matukio mbali mbali yanayoonesha utekelezaji wa Wizara ya Vijana, na Uwezeshaji Zanzibar




*Vijana wakiwa wenye furaha katika maadhimisho ya siku ya Vijana kimataifa 2025*



**Baadhi ya Picha za Matukio mbali mbali yanayoonesha utekelezaji wa Wizara ya Vijana, na Uwezeshaji Zanzibar**



*Ushirika wa Nia Safi wa Dunga Wilaya ya Kati Unguja ukiwa kwenye ziara ya kujifunza kilimo cha vitunguu Mkoa wa Morogoro.*



***Mhe. Shaaban Ali Othman**, Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji akikagua bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wa kituo cha Barefoot. Ukaguzi huo ni matokeo ya utekelezaji wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (ZEEA) katika kuwawezesha wananchi kiuchumi.*